


Kuelewa Huduma za Ustawi wa Watoto mu inchi ya Marekani kwa Vijana na jamaa Wakimbizi



Huduma za ustawi wa watoto ni nini?

Huduma za ustawi wa watoto ni huduma mbalimbali zenye zinasaidia kuchunga watoto salama na kusaidia jamaa wakati kuko wasiwasi kuhusu usalama ao malezi ya mtoto. Huduma za ustawi wa watoto ziko amo huduma za kuzuia matatizo, huduma za ulinzi wa watoto, malezi kwa muda mu jamaa ya malezi, na kuasili watoto.



Malengo ya huduma za ustawi wa watoto ni:

- Kuchunga watoto **salama**
- **Kusaidia** wazazi na walezi
- Kusaidia jamaa **kubakia pamoya** wakati wowote mambo iko salama
- Kuhakikisha kama watoto wanakomalia mu **nyumba zenye ziko amo usalama na utulivu**

Namna gani Huduma za Ustawi wa Watoto Zinaweza Kukusaidia

Msaada wa huduma za ustawi wa watoto mara mingi ni ya muda mufupi na inalenga kusaidia jamaa kupata utulivu na kubakia pamoya kwa usalama. Mara mingi, huduma zinaweza kuanza hata mbele ya tatizo kutokea, kwa kuunganisha jamaa na rasilimali za jamii, kutoa usimamizi wa kesi, na kusimamia kwa msaada wa masomo, banganga, na batu bengine benye banaaminiwa. Mipango za kuzuia matatizo zimeundwa kushugulikia changamoto mbele ya wakati, kutiwa jamaa nguvu, na kupunguza hitaji la huduma za msaada za zaidi. Huduma hizi za kuzuia matatizo mara mingi ni za hiari na hazihusishi Huduma za Ulinzi wa Watoto (CPS).



Huduma za ustawi wa watoto hazikusudiye kuwahukumu ao kupatia wazazi malipizi, wala hazitume mara moya kwamba watoto watoshwe mu nyumba zabo. Pia hazihusiane na ufuatiliaji wa sheria za uhamiaji. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za kuzuia matatizo zenye zinapatikana mu jamii yako, wasiliana na msimamizi wa kesi yako ao shirika lako la huduma za ustawi wa watoto la eneo.

Kuelewa Utoaji wa Habari wa lazima

Utoaji wa habari wa lazima inamaanisha kama kuko wataalamu wenye wanatakiwa kisheria kutoa habari kuhusu wasiwasi ya usalama wa mtoto kwa Huduma za Ulinzi wa Watoto (CPS)..

Hawa wataalamu wanaweza kuwa amo:



Wa limu na wafanyakazi wa masomo



Banganga, wauguzi, na wahudumu wengine wa afya



Wafanyakazi wa kijamii na wasimamizi wa kesi



Watoa hudumahuduma za malezi ya watoto



Washauri na wataalamu wa matunzo ya kisaikolojia



Maafisa wa kufuatilia sheria

Batu benye banahusika na utowaji wa habari wa lazima **banapashwa toa habari kwa CPS**. wakati bako na uhakika kama mtoto amenyanyaswa ao amezarauliwa. Habalazimishwe kuonyesha alama ya ukweli kama unyanyasaji imefanyika — banatakiwa tu kutoa habari kuhusu wasiwasi kusudi ichunguzwe na CPS.

- **Ya muhimu kukumbuka:** Utoaji wa habari wa lazima iko kwa ajili ya kuwalinda watoto.
- Kutoa habari kwa CPS ni njia kwa wataalamu ya kulomba msaada wakati banakuwa na wasiwasi kuhusu usalama wa mtoto.
- Ripoti haizoweyake tuma kunakuwa uchunguzi ao kutoshwa kwa mtoto mu nyumba yabo.

